

Huruma: Social Roles and Responsibility




FIGURE 16 Ustadh Mahmoud Mau reading *Mama msimlaumu* at the Jukwaani Festival in Nairobi in 2009; in his hand the newspaper report which inspired his composition

1 *Mama msimlaumu* (“Don’t Blame My Mother”)

Ustadh Mau wrote this poem in 2006 after finding an article in the *Taifa* newspaper about a dog rescuing an abandoned baby girl who had been left in the Ngong forest. The dog carried the baby to its owner, who at first thought that the baby was dead. Ustadh Mau reads the newspaper every day; touched by the baby’s story, he decided to write a poem about it to defend the rights of women, who are commonly blamed for such acts. He has performed the poem twice for audiences. Before reading the poem, he reads them the newspaper article and asks the audience, whom do you blame for such an act? Normally, he says, the audience blames the mother. His intention is to change people’s perspectives and to place the deed in a broader social context: not only the mother, but also society is to be held responsible.¹

1 On the occasion of the first conference on Swahili literature at the University of Naples, organ-

1. *Imenibidi kunena, kabla wangu wakati
Sababu nimewaona, mamangu humlaiti
Mamangu makosa hana, sipweke amezohiti'
Kosa hili nda ummati*

I have been compelled to speak prior to my time
Because I have seen you condemning my mother.
My mother is not the one to blame; it is not her fault alone.
It is society's fault.

I -hiti < Ar. syn.: *-fanya makosa* "make a mistake."

2. *Nda ummati hili kosa, na ziyongozi wa nti
Kosa nda wana siyasa, na mahakimu wa koti
Kosa nda wenye mapesa, na wasiyo na senti
Kosa hili nda ummati*

It is the fault of society, and the leaders of the country.
It is the fault of the politicians and the judges in the court.
It is the fault of those who have money and those without a cent.
It is society's fault.

3. *Mamangu si Mariyamu, wa Imrani binti
Mama ni mwanaadamu, meishi hapa tiyati
Na nyuteni mwafahamu, kuna dhaifu wakati
Hushindwa kuidhibiti*

My mother is not Maryam, the daughter of Imran.
My mother is a human being, living here on earth.
As all of you know, there are times of weakness
In which we fail to control ourselves.

4. *Mama hakutenda pweke, na labda hakukiri
Ali na mwendani wake, aloifanya jasiri
Ndipo mimi niumbike, mamangu kumuaziri'
Pasi na yangu khiari*

ized by Flavia Aiello and Roberto Gaudio in 2016, this poem was also read aloud, with a translation into Italian by Annachiara Raia under the title "Non incolpate la madre."

My mother did not do it alone, and probably not voluntarily.
 She had a partner who feigned adventurousness.
 That is how I came into being, putting shame on her—
 Against my own will.

1 *kumuaziri*—Mau: *kuntia katika aibu* (“to put shame on s.o.”).

5. *Ikiwa kuna lawama, lawama na zitanganye*
Mukimlaumu mama, naye baba mumkanye
1 Ndipo hapo yatakoma, ubaguzi musifanye
Wanawake musifinye

If there is someone to be blamed, this blame should be distributed
 equally.
 If you accuse the mother, the father also should be blamed.
 Only then can this be prevented; don't be biased
 And place the blame on women alone.

1 In this third line, he is referring to extramarital pregnancy. From his point of view, one can only stop men from dallying with women by making them legally responsible for their acts and not placing the blame solely on women, who thus become socially marginalized.

6. *Mimi kattu sikubali, mamangu kumlaumu*
Na pweke kumkejeli, huwa ni kumdhulumu
Kwaye pweke yambo hili, aswilani halitimu
Hilo nyute mwafahamu

I do not agree if you blame my mother
 And ridicule only her, because this is an injustice.
 She could never have done this by herself.
 You all know that.

7. *Kitendo ni cha wawili, alipowa kapokeya*
Haitokuwa adili, mama pweke kumwemeya
Halihitaji dalili, wala huja kuzengeya
Ayuwa kulla mmoya

This can only be done by two people: the one who received [the offer],
also accepted it.

It's unfair to place the onus only on my mother.

No evidence is necessary nor need any proof be found.

Everybody knows it.

8. *Mno huwona utungu, kiwasikiya hunena*
Humlaumu mamangu, kwa kuwa mkosa sana
Mimi na wendani wangu, hatupati hata ina
Ni Sina au Sibina

I feel so much bitterness if I hear people talking,

Blaming my mother as the only wrongdoer.

My fellow sufferers and I, we are not even named—

Only Sina or Sibina.¹

¹ These two names are telling: Sina, “I don’t have [sc. a father],” and Sibina, “it is not surprising,” i.e. “it is not a surprise that these things happen.” These are female names given to children who are born outside of wedlock.

9. *Menitupa wangu mama, si kwa kuwa hanipendi*
Ni baba memsukuma, kisa kumwawika landi'
Naye kwa kucha lawama, za wenye ndimi na tundi
Menitupa yake kandi

My mother threw me away, but not because she had no love for me.

It was the father who pushed her, putting the hangman’s noose around
her neck.

It was just from fear of being accused by scandalmongers and chatter-
boxes

That she threw me, her treasure, away.

¹ *landi* “noose”; *wenye tundi* (< -*tunda* “to find out”) “chatterboxes.”

10. *Naamini anipenda, mama hakunitukiya*
Ni lipi lilomshinda, pumzi kuniziwiya
Tokeya siku ya kwanda, duniani mimi kuya
Ni ruhuma kunoneya

I believe she loved me. My mother did not hate me.
 What else would have prevented her from suffocating me right away?
 From the first day I came into the world,
 She felt compassion for me.

11. *Natamani natamani, wangu mama kumpata
 Nimwambiye shukurani, nimpe ahasanta
 Kwa kunilicha tumboni, hata siku zikapita
 Ndiya nami kafuwata*

I wish, I wish, to find my mother,
 So that I can thank her and show her my gratitude
 For keeping me in her womb, until the time was due for me
 To find my way out.

12. *Humpijiya siloti, mamangu kwa wake wema
 Wakuniwata niketi, matumboni kwa salama
 Na wala simlaiti, kwa alilolifanya mama
 Alitenda kwa lazima*

I salute my mother for her kindness
 To let me stay safely in her womb.
 And I do not blame my mother for what she did.
 She was forced to do so.

1 *siloti* < Eng. "salute."

13. *Menitatiya tambara, kusudi kunidhibiti
 Nisipate la madhara, kiniweka kavu nti
 Baridi ingenikera, nikakutwa ni maiti
 Alofanya si katiti*

She wrapped me in a piece of cloth to protect me
 So that I would not be harmed when she placed me on the bare
 ground.
 For if the cold had struck me, I would have been found dead.
 What she did was not trifling.

14. *Kabla ya kumaliza, kufunga yangu kauli*
Walimwengu nauliza, tazawa mara ya pili
Hakuna takaoweza, kuwa wa mama badali
Nashukuru wafadhili

Before I finish and conclude my speech,
 I ask you human beings: can I possibly be born a second time?
 There is no one to replace my mother.
 Still, I thank all my saviors.

15. *Wema wenu siukani, na wa mbwa mashuhuri*
Mumenitenda hisani, mumenifanya mazuri
Wangaliko duniyani, waja wapendao kheri
Tammati hapa shairi

I cannot deny your kindness, nor that of the famous dog.
 You have done me a favor and you have done good to me.
 There are still people in the world who are altruistic.
 Here my poem ends.

2 *Jilbabu* (“Veil”)

Ustadh Mau composed this poem in the 1980s, when a group of women was campaigning for the proper veiling of Muslim women. They were of the opinion that women were not properly veiled, and they propagated the use of a (typically black) veil called the *jilbabu*, made of two parts: one piece wrapped around the hips, and another around the shoulders. This was supposed to replace the so-called *buibui ya Kiswahili*, which is one piece of cloth, sewn into a loop, and which women typically wore in a loose way. The “Annaswiha” movement was started mostly by women from Lamu who had studied in Nairobi, where they met other (mostly Somali) women and returned to Lamu with new ideas about proper clothing. Mama Azra, Ustadh Mau’s wife, was the chairperson of the group. The poem was also performed at Mkomani Primary School, where Ustadh Mau has given lectures on moral conduct (*maadili*) every Thursday (in the Islamic Pastoral Program) for decades, ever since the 8-4-4 school system was introduced. This is one of the poems in this collection that has a dialogical structure, based on a conversation between a young girl, called only *binti* (“daughter”), and her father, *baba*. As the poem unfolds, the reader can see that while the girl is curious and feels

ready to start wearing her veil, the father expresses his hesitation toward his daughter's wish.

1. *Binti:*
Babangu tangu kitambo
Kwako nalitaka yambo
Imekuwa kama nyimbo
Kula siku nakwambiya

Daughter:
 My father, for a while now
 I have wanted something from you.
 It plays on repeat in my head
 Every day, I tell you.

2. *Baba:*
Ewe binti sikiza
Mimi hilo sitoweza
Haja yako kutimiza
Sivezi kukutendeya

Father:
 My daughter, listen—
 I can't do that.
 I can't satisfy your need.
 I can't do it for you.

3. *Binti:*
Baba kituche¹ si ghali
Wala si cha mengi mali
Alifu na mia mbili
Hazizidi hata moja

Daughter:
 Father, this thing is not expensive;
 It is not a lot of money.
 One thousand two hundred—
 It is no more than that.

¹ *kituche = kitu hicho*

4. *Baba:*
Mwanangu hukufahamu
Mimi sioni ugumu
Wa kutowa tas'limu
Si bakhili kwa rupiya

Father:
 My daughter, you haven't understood me.
 I don't see any problem
 In paying;
 I am not a miser when it comes to money.

5. *Binti:*
Basi baba ni kwa nini
Kwamba haiwezekani
Ikiwa yake thamani
Siyo ilokulemeya

Daughter:
 So, father, why then?
 Why is it not possible
 If its price
 Is not the thing that prevents you?

6. *Baba:*
Mwanangu mimi naona
Hilo halina maana
Wewe ungalii kijana
Ni mwando kuinukiya

Father:
 My daughter, I see
 That this is not meaningful.
 You are still a child;
 You have only just begun growing up.

7. *Binti:*
Baba hela pulikiza
Suali nakuuliza
Wewe litakupendeza
Mimi mwano kipoteya
- Daughter:
 Father, listen
 To the question I am asking you:
 Would you want me,
 Your daughter, to go astray?
8. *Baba:*
Utapoteya kwa nini
Wewe hapa si mgeni
Hata usiku kizani
Ndiya zote zakweleya
- Father:
 Why should you go astray?
 You are not a foreigner here.
 Even on the darkest night,
 You know all the roads.
9. *Binti:*
Si kupoteya ndiyani
Ni kumwandama shetani
Ni kungiya madhambini
Kutenda yaso na ndiya
- Daughter:
 I do not mean getting lost on the road,
 But following Satan.
 It means to sin—
 To do what is not right.
10. *Baba:*
Hilo mimi silitaki
Na kabisa siridhiki
Mambo yaso alaiki
Kwetu hatukuzoeya
- Father:
 I don't want that.
 And I do not agree at all with
 These things that do not befit us,
 That we are not used to.
11. *Binti:*
Kama hayo wayaona
Ni mambo yaso maana
Nipa ningali kijana
Nipate kulizoeya
- Daughter:
 If you think
 That these concerns are meaningless,
 Expose me to them while I am still young,
 So that I may get used to them.
12. *Waswahili twalinena*
Uwongo^I hupatikana
Ulimai^{II} na mwenana^{III}
Uweze kusinyangiya
- We, the Swahili, used to say
 The clay
 Needs to be wet and soft
 So that you can model it.

^I *uwongo* Am. "clay" (Std. *udongo*). | ^{II} See meth.: *uwongo hupatikana ulimai*. | ^{III} *mwenana* "kitu laini, kitu ambacho hakijakomaa" (Mau).

13. *Nami kitovaa sasa*
Wakati utapotasa
Sitoliweza kabisa
Kiwa sitolizoweya If I am not wearing it now,
When the time comes
I will not be able to wear it at all,
If I do not get used to it now.
14. *Baba:*
Mwana hilo si lazima
Bora usimame wima
Ndiya njema kuandama
Na mbovu kuikimbiya Father:
My daughter, this is not a must;
You better stand firm,
Following the right path,
Running away from evil.
15. *Binti:*
Baba shuga ndiyo kinga
Na waovu hukutenga
Baba kitovaa shuga
Mate watanimiziya Daughter:
Father, the veil is a protection.
It keeps one away from bad people.
Father, if I do not wear a veil,
They will desire me.
16. *Kizunguka wazi wazi*
Kuna wengi majambazi
Wabakaji siku hizi
Miini wameeneya If I stroll around without it—
There are many robbers
And rapists these days.
They have increased in the towns.
17. *Lakini kiisitiri*
Kama ya Mola Amri
Nitaepuka khatari
Salamani nitangiya But if I cover myself
According to God's will,
I will avoid danger
And be on the safe side.
18. *Baba:*
Basi enenda dukani
Kaangalie fesheni
Zitokazo Arabuni
Nipate kununuliya Father:
So go to the shop
And look at the fashions
Coming from Arabia,
So that I may buy it for you.
19. *Binti:*
Baba shuga si fesheni
Mashuga ya madukani
Siyo kwenye Qurani
Mola aliyotwambiya Daughter:
The veil is not a fashion item.
The veils from the shops
Are not those of the Qur'an,
Which God told us about.

1 *shuga* Am. "sheet," here "veil" (Std. *shuka*)

20. *Baba:* Father:
Kwani wewe utakalo Which one do you want?
Ni lile liambiwalo Like the one called
Junijuni' hilo ndilo "This is Junijuni"
Kwa mbali akitokeya When s/he appears from afar?

1 In this stanza, *junijuni* refers to a figure that forms part of a children's game typically played during Ramadan. A rough bag is placed over a child's head so that s/he cannot see anything. Afterwards, other children make fun of him/her, shouting "Junijuni lataka bembe" ("Junijuni wants *bembe* food"). (*bembe* food is a kind of food consumed during Ramadan.) Thus, in this stanza, the father makes fun of the daughter's wish, since the *junijuni* is an ugly bag. It has become a common derogatory term, used to refer to the veil by those who do not approve of it.

21. *Binti:* Daughter:
Baba sifanye dhikaka Father, do not joke—
Hilo ndilo la hakika That one is the right one,
Mola analolitaka The one God wants,
Shuga analoridhiya The one God agrees with.
22. *Amri yake Wahabu* The command of the Generous One
Ni kuvaa jilbabu Is to wear the veil.
Angaliya ah'zabu Look at the *Sūrat al-Aḥzāb*—
Imenena wazi aya The verse says so clearly¹.

1 The reference is to sura 33:59, which reads as follows: "O Prophet, say to thy wives and daughters and the believing women, that they draw their veil close to them; so it is likelier they will be known, and not hurt. God is All-Forgiving, All-Compassionate" (Abr., 434).

23. *Baba:* Father:
Mwanangu nasikitika My daughter, I am sorry.
Wendiyo watakuteka Your companions will laugh at you,
Na kwa joto kadhalika And the heat
Utazidi kuumiya Will make you suffer even more.
24. *Binti:* Daughter:
Kitekwa siandi mimi I am not the first to be laughed at.
Hata wake wa mitumi Even the Prophets' wives
Walikiliwa kwa ndimi Were slandered
Na kuzuliwa mabaya And defamed¹.

1 See for instance Qur. 24:2.

25. *Ama kunena ni joto* And as for the heat,
Joto ni kitu kitoto Heat is a minor thing
Kuliko akhira moto Compared to the hellfire
Mtu kwenenda kungiya One will be thrown in.
26. *Baba:* Father:
Mwanangu umenishinda My daughter, you have defeated me
Hoja zako kuzivunda With your counterarguments;
Ingawa nimeipinda Though I made an effort,
Sikuweza hata moyo I did not succeed, not even once.
27. *Kalishone jilbabu* Go and sew your veil.
Uvae wangu muhibu Wear it, my beloved daughter,
Kwani radhi za Wahabu Since it is necessary
Yapasa kuzizengeya To seek to please God.
28. *Binti:* Daughter:
Nakushukuru babangu I thank you, my father,
Kunikubaliya yangu For giving me your permission.
Hini amri nda Mungu This is God's order;
Ndiye amezotwambiya He is the one who told us so.

3 *Mchezo wa kuigiza* (“Play”)

This is a poem in *wimbo* form that Ustadh Mau composed in 2011, and his daughter Azra Mau prepared the first translation, which we have revised here. It was inspired by a prose version of the same story that he read in an Arabic textbook for class six in Saudi Arabia, where the story bore the title *Bayna al-ghanī na al-faqīr* (“Between the Rich and the Poor”). Because he liked the content, he decided to adapt it to poetic form in Swahili. He presented his adaptation to his own pupils at the madrasa as a poetry exercise for reading and comprehension. As in the poem *Jilbabu*, this poem is one of several composed in the form of a dialogue, a “play” (*mchezo*) in verse form. In the play, the two voices—that of the Miser, on the one hand, and the Pauper (also referred to as “Shekhe”), on the other—are not rounded characters, but are allegories of richness and poverty. They represent groups defined by their socioeconomic differences and their outlooks—in the form of the miser and the poor man—rather than individuals. This dialogic form allows for an exchange of arguments to finally arrive at a conclusion that includes the moral message that the audience should keep in mind.

1. *Bakhili:*
Mali yangu, mimi nakupenda sana
Wewe kwangu, hushinda mke na wana
Nautungu, kwako mwingi nauwona

Miser [addressing his wealth]:
 My wealth, I love you so much.
 You are better than my wife and children.
 I suffer so much for you.

2. *Yangu raha, ni mali kuyatizama*
Si mzaha, haya ninayoyasema
Ndiyo jaha, kwenye duniya nzima

My pleasure is looking at my wealth.
 It's not a joke, what I am saying:
 This is the greatest joy in the whole world.

3. *Masikini:*
Ewe bwana, tajiri mwenye nafasi
Tangu yana, mimi riziki siisi
Hela fanya, hisani wema hukosi

Pauper:
 O master, rich man who can afford a lot,
 Since yesterday I have not eaten.
 Please, do me a favor, and you will not lack any blessing.

4. *Ukinipa, na mimi kitu katiti*
Takulipa, Mola ziviye senti
Tangu hapa, na baada ya mauti

If you also give me a little bit,
 God will pay you, your savings will grow
 Here in this world, and also after death.

5. *Bakhili:*
Enda zako, sinitiliye nuhusi
Haja yako, wataka zangu fulusi
Na sumbuko, nilopata huliisi

Miser:

Go away; do not bring me bad luck.
Your wish [is that] you want my money,
But you don't know the troubles I have endured.

6. *Nondokeya, sisimame mbee yangu*
Takutiya, cha kitwa hiki kirungu
Nakwambiya, kutowa mali utungu

Disappear from my sight; do not stand before me.
I will hit you on the head with this club.
I am telling you, giving money away is painful.

7. *Masikini:*
Mabakhili, wenye mali huteseka
Yao hali, ni kama sisi hakika
Kula hali, ni mali huyarundika

Pauper:

Misers who have wealth are in trouble.
Their state is just like ours:
They do not eat; instead, their only ambition is to amass wealth.

8. *Hufaani, zake nyingi miliyoni*
Masikini, hawafanyii hisani
Zibengini, mwenyewe huzitamani

How are his millions of any use to him?
To the poor, they are of no benefit;
They just stay in the bank, because the owner wants them there.

9. *Shekhe:*
Hodi bwana, ewe nduyake Karuni¹¹
Nimeona, nikutowe uwingani
Wakusanya, mali wamwekeya nani

Sheikh:

Hodi master, oh brother of Karuni,
I thought that I had helped you out of your ignorance.
You are collecting wealth, but for whom are you saving it?

1 *hodi* a call-word used by someone outside the door who wants to enter a house; similar to knocking at someone's door. | 11 The rich tyrant Qarun, who appears in the Qur'an, sura 28:76–84, is the prototypical careless and powerful man who is interested solely in high rank and wealth, exploiting others. He does not think about the afterlife, but merely tries to accumulate as much wealth and status as he can in this world. There is also a reference to him in stz. 100 of the poem *Hapo zamani za yana*.

10. *Angaliya, mali mengi umeweka*
Zingatiya, kuna wengi huteseka
Wanaliya, kwa kuwazidi mashaka

Look, you have kept a lot of wealth;
 Consider how many people are suffering.
 They are crying in their great sorrow.

11. *Mayatima, waliokosa mababa*
Kina mama, wasokua na akiba
Fanya hima, uwape japo kibaba

Orphans who have lost their fathers,
 And mothers who have no savings—
 Make an effort; at least give them a dime.

12. *Na maradhi, wangine huwasumbuwa*
Na baadhi, hamudu kupata dawa
Mwenye hadhi, towa utabarikiwa

And sickness: some are afflicted by it,
 And some cannot even afford to buy medicine.
 Oh, you of high honor, donate and you shall be blessed.

13. *Bakhili:*
Yangu mali, ndiyo wewe wayataka
Si kauli, hiyo uliyotamka
Na akili, nadhani imekuruka

Miser:
 My wealth, that is what you want.
 It is not proper, what you have just said,
 And I think you are out of your mind.

14. *Wanekeza, mimi kutowa sadaka*
Nimeiza, sitaki na sitotaka
Nitasoza, shauri lako kishika

You tell me to give alms;
 I refuse—I do not and shall never want to.
 I will perish if I take your advice.

15. *Wanidhiki, kwa maneno ya upuzi*
Siyataki, hayo yako siyawezi
Sigeuki, mali yangu sipotezi

You are annoying me with your useless words.
 I do not accept them; I cannot stand them.
 I will not change; I shall not lose my wealth.

16. *Nitokeya, nyumbani kwangu haraka*
Nondokeya, usisimame dakika
Yako niya, ni mimi kufilisika

Get out of my house quickly.
 Vanish; do not stand before me, even for a second.
 Your intention is to bankrupt me.

17. *Shekhe:*
Umekosa, walodhani wewe siyo
Zako pesa, siyo mimi nitakao
Takutesa, ufahamu siku hiyo

Sheikh:
 You have erred; what you think is not true.
 Your money is not what I want;
 It will burden you, remember, on Judgment Day.

18. *Mepofuka, wewe kwa kupenda mali*
Kuongoka, kwako ni kama muhali
Takumbuka, kiadiya zilizali'

You are blinded by your love of wealth.
 Becoming righteous is not possible for you—
 You will remember when the earthquake comes, right on time.

I zilizali “earthquake.” This too is a reference to Judgment Day, when the earth will tremble (see also sura 99).

19. *Yako dini, umetupa kwa duniya*
Na motoni, maliyo yatakutiya
Mayutoni, siku hiyo^t tasaliya

Your religion: you have given it up for love of this world.
 It is into hellfire that your wealth will throw you;
 You will remain in regret on that day.

I siku hiyo “that day,” another reference to Judgment Day.

20. *Mali yako, yatakuwa ndizo kuni*
Nyama yako, yakiiyoka motoni
Nasumbuko, likikutesa mwendani

Your wealth will be firewood in hell;
 Your flesh will be roasted in the fire,
 And pain will put you in agony, my friend.

21. *Bakhili:*
Tumo langu, la nyezi nyingi na nyaka
Ruhu yangu, ile ndiyo huchomeka
Bure yangu, bure nalihadaika

Miser:
 My savings of many months and years are gone—
 And my soul is burning.
 Alas, for nothing, I have been deceived!

22. *Yamekwenda mali, mebaki mayuto*
Zote zanda, huuma kiliya mato
Imevunda, jahazi ya langu pato

My wealth has disappeared; only regrets remain.
 I bite my nails in regret, crying many tears.
 It has been broken, the dhow that brought me my income.

23. *Laitani, nangalikula vizuri*
Muilini, kavaa nikanawiri
Ni shetani, ndiye aliyonighuri

If I had known, I would have eaten well;
 I would have put shining clothes on my body.
 It was Satan who deceived me.

24. *Masikini:*
Tulingene, tumekuwa hali moya
Na lingine, huna lililosaliya
Twandamane, tushike moya ndiya

Pauper:
 We have become equals; we are in the same state.
 Anything else? You have nothing that has remained.
 Let us walk together; we take the same path.

25. *Hafaidi, mtu bakhili kwa mali*
Ni hasidi, mwenyewe kwa yake hali
Akizidi, humrusha na akili

He will not derive any benefit, a miser saving his wealth.
 He is envious; he does not allow anything, even to himself.
 If he overdoes it, it can even make him lose his senses.

4 *Haki za watoto* (“Children’s Rights”)

Ustadh Mau wrote this 257-stanza poem in May 2001. At the time, his last-born son, Aboud, to whom he dedicated the poem, was three years old. In total, Ustadh Mau has eleven children from two wives, as well as thirty-four grandchildren. His first wife, Mama Tunda, gave birth to three girls and five boys. The second wife, Mama Azra, gave birth to two girls before finally giving birth to Aboud. According to Ustadh Mau, he composed the poem after having read various books in English and Arabic on childcare and developmental psychology. He gradually became aware of children’s special needs and concerns. He recognized his own failures, misconceptions, and mistakes, as well as problems in society at large. Furthermore, according to him, his first wife was too rude toward the children, while his second wife was very dedicated to her work. She first worked as a schoolteacher and later at the Lamu Museum, so she did not have much time for the children. Ustadh Mau says that he was very close with the children. As he recounts, even at the hospital, the nurses would give the babies to him so that he could hold them. Even nowadays, his grandchildren always come to his library, where they get sweets or some small coins from him.

Ustadh Mau himself was brought up by his paternal uncle. He has five siblings. All the others were brought up by his mother and their father. But since his uncle’s children did not survive, his father decided to give Mahmoud to his uncle to raise him. His uncle treated him well; he was never beaten, in contrast to many other children at the time. He also arranged for his education and made him study. His wife was well learned in the Qur’an, so Mahmoud already knew how to read the Qur’an before starting school.

Furthermore, Ustadh Mau is also a teacher, and loves to teach children at the madrasa. He is a member of the committee (*wizara*) for children’s rights in Lamu, which now seems to be largely defunct. Previously, he also used to be called to court if there were cases of child abuse or, in cases of divorce, when a father would not provide for his children.

On the one hand, the poem is also a didactic and personal poem, a *wasiya* dedicated to his son Aboud—like the one Ustadh Mau’s father composed for him (see *Hapo zamani za jana*). On the other hand, the poem is not a typical *wasiya*, addressing children and advising them on how to live in the world. Rather, it speaks to a wider audience, and more particularly the parents, not



A recorded audio version of the poem is freely available online at <https://doi.org/10.6084/m9.figshare.20200514>.

the children. His concern for the children and his way of addressing the parents has been noted as quite unusual by his Lamuan audience, since typically it is the children who are taught through such poems.

In the poem, he makes a plea to treat children based on their needs and rights (see also Vierke's contribution "How Ought We to Live?" in Part 1 of this volume). He systematically goes through various elements of children's life-worlds, progressing by age group. He starts by considering babies and infants before moving on to children and adolescents. Later in the poem, he makes a plea for educating children properly, which reflects his general concern with proper education as the key to individual and societal progress. The media in particular has a bad influence on children in his view: it makes children go astray and lose interest in studying. In the poem, he does not refer to social media or the internet, as in 2001, the former did not exist and the latter hardly played a role in everyday life in Lamu. In the context of the poem, it is TV that he is condemning: satellite TV, which came with many additional channels, arrived in Lamu in the 1990s. According to him, the TV programs not only caused children to lose focus on their studies, but also introduced them to harmful content.

- | | | |
|----|--|--|
| 1. | <i>Bismillahi Latwifu</i>
<i>Kwa ina lake tukufu</i>
<i>Naanda kuyaswanifu</i>
<i>Ya Rabbi nitimiziya</i> | In the name of God, the Kind One,
In His glorious name,
I begin composing.
May you, God, help me complete this! |
| 2. | <i>Nitimiziya yatimu</i>
<i>Rabbi niliyozimu</i>
<i>Nieleze wafahamu</i>
<i>Watakao kusikiya</i> | God, make it complete,
What I intend to compose,
So that I can reach
Those who listen to my words. |
| 3. | <i>Shabaha na langu lengo</i>
<i>Nataka tunga utungo</i>
<i>Asaa uziwe pengo</i>
<i>Kwenye maudhui haya</i> | My target and my aim
Is to compose a poem;
Maybe it can fill a gap
When it comes to this topic. |
| 4. | <i>Nitakayo kuyanena</i>
<i>Ni mambo kuhusu wana</i>
<i>Khususwa walo wanuna</i>
<i>Haki zao za shariya</i> | What I am about to say
Concerns children,
Especially the young ones:
It is about their legal rights. |

5. *Haki za walo watoto* The rights of those who are young
Ni kuu mno si toto Are essential and not minor,
Zimepowa na uzito And religious and secular laws also
Kwa dini kanuni piya Grant them importance.
6. *Nami tatiya mkazo* And I also emphasize their rights
Kuzitaya haki hizo By mentioning those
Kwenye shariya ambazo Of the sharia laws that
Mola amewapangiya God has put in place for children.
7. *Tazizungumza haki* I will talk about the rights
Alizowapa Khallaki That the Creator has bestowed on
Hawa wana makhuluki Children created by Him
Kwenye hadithi na aya Through the hadith of the Prophet and the
 Qur'ānic verses.
8. *Hadithi sitoandika* I will not quote the hadith
Aya sitoazitamka Nor recite the verses,
Muwanga wake hakika But certainly they enlighten
Ndiwo taomulikiya My perspective on the topic.
9. *Uislamu ni dini* Islam is a religion
Mno inayothamini That values
Wana tangu matumboni Children, from the time they are in the
Bali kabula kungiya womb
 And even before their conception.
10. *Ni haki ya alo mwano* It is the right of your child
Kumpa mama mfano To have an ideal mother,
Aliyo mzuri mno Who is excellent
Si kwa sura kwa tabiya Not in appearance, but in character.
11. *Kabla ya kuamuwa* Before deciding
Ni upi wa kumuowa Whom you will marry,
Upike ukipakuwa' Consider it carefully
Mama mwema kwangaliya And look for the qualities of a good mother.

I *upike ukipakue* idiomatic for “consider carefully”; as Mau notes (*ufikirie sana, kwa maki-ni*), literally “cook [your thoughts] before you serve them.”

12. *Ni lazima ufikiri*
Mambo yatakayojiri
Kiwatunuku Qahhari
Wana akawaptiya You should try to imagine
How things will be
If the Powerful One rewards you
With children.
13. *Fikiri uwaze mno*
Kuhusu mama wa wano
Usiwe wako mkono'
Kizani utautiya Ponder carefully
The mother of your future children;
Don't select her hastily
Or blindly.
- i -tia mkono gizani* "to do something without first thinking about it."
14. *Usiutiye kizani*
Kwa kuteuwa mwendani
Alokungiya matoni
Moyo wako kavutiya Don't choose blindly
By selecting a partner
Who attracted you at first sight
And seduced your heart.
15. *Mama mno ni muhimu*
Taka mama alotimu
Wana wasikulaumu
Mambo takapo weleya The mother is very important.
Look for a perfect mother
So that the children will not blame you
When they reach the age of understanding.
16. *Mteuwe mama bora*
Si kwa kabila na sura
Bali ni kwa njema sera
Mwenye dini na tabiya Choose the best mother,
Not for her tribe nor for her beauty,
But for her good conduct
In religion and etiquette.
17. *Wape mama wa fakhari*
Mwenye mayezi mazuri
Wanao waifakhiri
Kwa mama kuivuniya Give them an admirable mother
Who can raise them well,
So that your children can be proud
Of their mother.
18. *Siwape mama mtango'*
Na mwenye tabiya jongo
Hoyo tawatiya pengo
Ya milele kusaliya Don't give them a mother who likes to stroll
about,
One with a bad character;
She will leave a hole
That will remain forever.

i mtango < -tanga "to stroll about." "Se promener de long en large, errer ou aller çà-et-là, à l'aventure de côté et d'autre; vagabonder." (Scl. 866).

19. *Wape mama mtulivu* Give them a calm mother
Asiyo mtepetevu Who is not idle,
Muyuzi alo mwerevu But knowledgeable and smart—
Si mama wa kuukiya And not a mother who likes to shout.
20. *Alokomaa akili* Someone who is mature;
Aso mengi mashughuli Who is not too busy,
Tawatunga kwelikweli But will truly look after
Wana na kuangaliya And take care of your children.
21. *Ni bora kiwa mesoma* It is better if she is educated,
Wala sambini lazima But I do not say this is a must—
Kwani alosoma mama Because an educated mother
Ni mengi yatamweleza Understands a lot more.
22. *Mama akiwajibika* If she is concerned about them,
Na wana hunufaika The children will benefit,
Na mambo mengi hunyoka And many things will go well
Yakandama sawa ndiye And take the right course.
23. *Kwani mama ni mwalimu* Because a mother is
Wa kwanda mno muhimu A child's first important teacher.
Athariye nda kuudumu She makes a lasting impact
Kwa wanawe husaliya On her children.
24. *Kiwata athari njema* If she has a good influence,
Itasaliya daima It will always remain.
Na piya mbovu alama Likewise, negative impressions
Hayondoki hubakiya Don't disappear, but remain.
25. *Nimeyafanya marefu* I've elaborated extensively
Ya mama kuwaarifu Upon the qualities of a mother:
Mama kiwa mwuongofu If the mother is virtuous,
Huongoka na dhuriya The children will be too.
26. *Ya pili haki ya mwana* The second right of a child
Kizawa handikwa ina Is to be given a name after birth:
Binti au kijana Girl or boy,
Lake la kukusudiya Children should have their own name.

27. *Ina haandikwi lolote*
Ni haki yake apate
Ina kama wende wote
Ambalo tafurahiya Children should not be given just any name:
 It is their right to have a name
 Like all other children,
 One that will make them happy.
28. *Simwandike ina ovu*
Kwake itakuwa kovu¹
Na ya moyo maumivu
Siku zote tasikiya Don't give them a bad name
 That will remain like a scar
 And cause pain in their heart
 Every time they hear it.
- ¹ *kovu* "scar." "Cicatrice, balafre; *Mwenye k.*, balafre. *Mtu wa makovu-kovu*, personne toute couverte de cicatrices" (Scl. 443).
29. *Mpe ina lilo zuri*
Kwa wende aifakhiri
Kuitwa awe hajeri
Bali huliteremeya Give them a good name,
 To be proud of around other children—
 When called, they will not be ashamed
 But be happy about it.
30. *Ni haki kumwandikisha*
Mwana kumuorodhesha
Sive tamuhangaisha
Sikuze zikiadiya It is their right to be documented,
 To be listed in the census,
 So that it will not cause them trouble
 In the future.
31. *Ni haki kumsajili*
Rasmi kwa sirikali
Wanawake na wavuli
Ni haki kwa wote piya It is their right to be registered
 Officially at the local administration.
 Girls and boys alike—
 It is the right of each of them.
32. *Hili yambo ni muhimu*
Kwa watu wote fahamu
Nawe usione wumu¹
Mwanao kumwandikiya This issue is important
 For everyone, understand—
 Don't think that it is difficult
 To register your child.
- ¹ *wumu* Am. "hardness" (Std. *ugumu*)
33. *Mmwandikiye karatasi*
Mwano kizawa upesi
Usipoteze nafasi
Kisa utaiyutiya Have a certificate issued
 Right after the birth of your child;
 Don't waste any time,
 Otherwise you will regret it later.

34. *Kitoandika haraka* If you don't get them registered early,
Hata mwano katukuka And wait until they are grown up,
Ni mno utasumbuka You'll have great difficulty
Baadaye kuzengeya Getting it later.
35. *Ni haki kulla mwanati* It is the right of every citizen
Kizawa kupowa cheti To have a birth certificate;
Khaswa kwa wetu wakati Especially nowadays,
Ni dharura mambo haya This is necessary.
36. *Ni haki yake kupendwa* It is their right to be loved,
Na kwa mapenzi kuundwa To be brought up with love:
Wazazi wengi hushindwa Many parents fail
Haya kuwatimiziya To do this.
37. *Wana wahitaji hili* Children need
Mapenzi ya kwelikweli A lot of love.
Mapenzi na maakuli Between love and food,
Mapenzi hutanguliya Love comes first.
38. *Tuwaoneshe ruhusa* Let us show them softheartedness
Na kuwapenda daima And let us always love them;
Kwa wote baba na mama Children demand this
Wana hili huzengeya From both father and mother.
39. *Tuwaoneshe imani* Let us show them kindness;
Twambe nao kwa makini Let us talk to them gently.
Tusizowee wendani Let us not adopt the bad habit, my friends,
Wetu wana kurukiya Of shouting at our children.
40. *Wana wakiwa wanuna* When the children are still small,
Hilo hawapendi sana They don't like this at all.
Akiukiwa huwona When they are shouted at, they feel
Ni mno memuoneya That you are abusing them.
41. *Wana wakizungumza* When children address us,
Yataka kuwasikiza We should listen to them.
Wana tukiwapuuza When we ignore them,
Huwapa fikira mbaya We make them feel bad.

42. *Wana na tuwasikize
Watakayo watweleze
Wana na tusiwapuze
Hiyo si njema tabiya* Let us listen to our children
And let them explain to us what they want.
We should not neglect them;
This is not a good habit.
43. *Tukiwapuza zijana
Huwavunda moyo sana
Ni dharura wakinena
Akilini kuwatiya* If we neglect the children,
We discourage them greatly.
It is a must to pay attention
When they talk to us.
44. *Na wana wetu tuteze
Kwa ziswa tuwapumbaze
Mazoweya tuyakuze
Na kwao kukaribiya* Let us play with our children;
Let us entertain them with stories.
Let us build good bonds
And let us be close to them.
45. *Wana na tuwakumbate
Yuuyuu tuwangate
Tuwaoneshe ya kite
Mahaba na mazoweya* Let us hug them,
And let us carry them high on our shoulders.
Let us show them unconditional love,
Affection, and closeness.
46. *Tuwape wana wakati
Sisi na wao tuketi
Tunene yapo katiti
Tashamiri mazoweya* Let us dedicate time to our children.
We should spend time with them;
Let us talk to them, even if it is only for a short while,
To strengthen our bonds.
47. *Tuwape wana nafasi
Wao kuteza na sisi
Kusudi nao wahisi
Hisabuni huwatiya* Let us give them a chance
To play with us
So that they feel
They are taken seriously.
48. *Tuwabusu wana wetu
Ni sunna ya tumwa wetu
Tangu zingali zitutu'
Mpaka kuinukiya* Let us kiss our children:
This is according to our Prophet's rules,
From the time when they are still small
Until they grow up.

1 *kitutu* (pl. *zitutu*) Am. "small child" (Std. *mtoto mdogo*; pl. *watoto wadogo*)

49. *Tungayaona matoto* Even if we think this is of minor importance,
Yana ndani na ukweto' These things run deep.
Athariye ni mzito Their impact is great:
Hayondoki hubakiya They do not vanish, but linger.
- I *ukweto* "depth."
50. *Wana haya wapatao* The children who experience this
Si sawa na wakosao Are different from those who don't;
Hawafani wana hao They do not resemble each other
Kwa nyendo na kwa tabiya In behavior or character.
51. *Wana haya wakipata* When children receive this,
Hukuwa pasi matata They grow up without difficulties,
Akili humetameta With bright minds
Kimawazo hutuliya And mentally stable.
52. *Mwana haya akosapo* If a child lacks this,
Kasoro nyingi huwepo There will be deficiencies:
Wana hunenda mapopo Those children go astray;
Hawandami sawa ndiya They don't follow the right path.
53. *Ndipo wawapo wakora* That is how they become troublemakers
Wazazi wakawakera Who upset their parents.
Tewengo' mara kwa mara Trouble again and again—
Na hawatindi udhiya They don't stop causing problems.
- I *tewengo* Am. "trouble" (Std. *maudhiko*)
54. *Mwana mapendi kikosa* If children lack love,
Enga mte kutonosa' They are like a seedling that is not watered.
Ukitokufa kabisa If they do not die,
Utasononeka¹¹ ghaya They will suffer a lot.

I -*nosa* Baj. = -*nosha* Am. "to water" | II -*sononeka* "to suffer" (Mau: *kutokuwa na raha* "to be without happiness")

55. *Atasononeka mno*
Kikosa mapendi mwano
Hono wa mte mfano
Zidi kuufikiriya They will suffer a lot,
If your children lack love.
Take the example of the seedling,
And keep pondering it.
56. *Mwana kitokwisa mwako*
Kupata mapendi yako
Huwa hesi babaiko
Kwenye moya kutuliya If children do not quench their thirst
For your love,
They will not be able to stop worrying
And calm down.
57. *Hatui hatamakani*
Hastakiri nyumbani
Na hata penye wendani
Mara huzuwa balaya The children will not be calm and settled;
They will not find comfort at home,
And even among their friends
They will suddenly pick quarrels.
58. *Huwa kama ibilisi*
Au kama mwanachisi
Zikiri¹ kwake hazisi
Kitinda handa zipiya [Such children] are like the devil,
Or like the bastard who is also the child of a
bastard.
Their misdeeds never end,
As soon as they stop, they begin again.
- ¹ *zikiri* Am. "mischief" (Std. *vitimbi*)
59. *Hayo yote ni athari*
Ya alopata dothari
Ya makosa yalojiri
Muda wa kuinukiya This is all the result
Of their experiences of being stigmatized
And being mistreated
In early childhood.
60. *Basi natutahadhari*
Tuwepuwe na khatwari
Wana tuyee uzuri
Bila kuwakaripiya So, let us be careful:
Let us protect them from danger.
Let us bring them up well
Without mistreating them.
61. *Na haki nyingine tena*
Alo amuru Rabbana
Ni kula kwa wetu wana
Kurwa na kuvaa piya And our children also have a right,
According to God's command,
To be nourished
And dressed.

62. *Mwana akisa kuzawa
Ni haki yake kupowa
Ya kushibisha maziwa
Kwa amri ya Jaliya* When a child is born,
It is the child's right
To be fed with enough milk:
This is the order of the Magnificent One.
63. *Maziwa haswa ya mama
Mwana kunwa ni lazima
Ya mamake yakikoma
Ya ng'ombe husaidiya* Especially mother's milk,
The child needs to drink.
If the mother's milk dries up,
That of the cow will help.
64. *Maziwa ya mama yake
Ni dharura kuu kwake
Akishiba kwayo pweke
Huwa na njema afiya* The mother's milk
Is of the utmost priority.
If children drink only this milk,
They will stay in good health.
65. *Wala sipende kumpa
Mwana maziwa kwa tupa
Dakitari huzitupa
Hawapendi kusikiya* Don't prefer to feed your baby
With milk from the bottle.
Even doctors throw this away;
They do not like to hear of it.
66. *Tupa si chombo kizuri
Ina na nyingi khatari
Mwana hesi utiriri
Tupa akiizoweya* The bottle is not a good container:
It brings many dangers.
Children do not stop whining
If they get used to bottles.
67. *Na tupa husababisha
Maradhi na hurarisha
Si sahali kuiyosha
Burashi unatumiya* And the bottle causes
Sickness and diarrhea;
It is not easy to clean it,
Even if you use a brush.
68. *Sharuti kuichemsha
Na kisa kuikausha
Mwana hukubabaisha
Lini utatenda haya* You have to boil
And dry it
While your child is fussing.
How will you manage all this at once?
69. *Tena ya mama maziwa
Ameyaumba Moliwa
Si moto hayakupowa
Ni tayari kutumiya* Furthermore, the mother's milk
That God has provided
Is neither too hot nor too cold,
But ready for consumption.

70. *Hayana nyingi harara*
Si baridi ya kukera
Mwana hukuwa imara
Ya mama akitumiya It is neither too hot
Nor harmfully cold;
Children grow strong
If fed with mother's milk.
71. *Yameumbwa kwa kipimo*
Haja zake zote zimo
Hakuna kiso kuwemo
Madini sukari piya The milk is well balanced
And provides for all their needs.
There is nothing lacking;
It contains minerals and sugar as well.
72. *Huhitaji kuyaonda*
Wala kudara kwachanda
Popote unapokwenda
Huwa na wewe pamoja You do not need to taste it,
Nor use a finger to test its temperature;
Everywhere you go,
You have it with you.
73. *Huwa ndani mwa matiti*
Tayari kula wakati
Mwana taabu hapati
Na mama huna udhiya It is in the breasts,
Ready at any time;
The child does not need to suffer,
And you, mother, are never in trouble.
74. *Kuyasahau huwezi*
Wala hayakupi kazi
Kimwakiza mitilizi
Huwa ichandama ndiye You cannot forget it,
And it does not cause much work.
As soon as you put the baby to your breast,
the milk starts to flow
And finds its way.
75. *Wala hayana gharama*
Kununuwa si lazima
Neema yake Karima
Wana amewaekeya It does not bear any cost;
You do not need to buy it.
The Generous One, in His bounty
Has provided it for the children.
76. *Basi kwani kuwawasa*
Wana wetu kuwamsa
Kab'la ya mwida kwisa
Kwa urembo kutapiya So why do you deprive them,
Weaning our children
Before the time has come¹
Out of fear of losing attractiveness?

¹ In the Islamic context of Lamu, it is common to breastfeed children for two years.

77. *Mamama huwadhulumu* The mothers inflict harm
Wana pasi kufahamu On their children unconsciously,
Ati ujana udumu Believing their youth should remain,
Yasimeme kusaliya And keeping their breasts' form.
78. *Mwana piya kadhalika* Likewise, it is the right of children
Ni hakiye kumpeka To be taken to the clinic
Kwa tarikhi kutochoka Regularly, without their parents tiring of it,
Kupima kudunga piya So that they may be vaccinated and
weighed.
79. *Mpeke chanjo apate* Take them to be vaccinated
Na ratiba afuwate Following the schedule.
Sindano moya siwate Don't miss even one vaccination;
Ni muhimu kutumiya It is important to get them.
80. *Usidharau sindano* Don't neglect the injections
Za ziweo na mikono In the thighs and arms;
Ni kinga hizo kwa mwano They protect your children
Muwili husaidi ya And help their bodies.
81. *Mwana umpe chakula* Give your children food
Na palo pema kulala And a proper place to sleep.
Ni hakize kwa jumla In sum, these are the rights
Sisi mbwa kuwatendeya We should provide for them.
82. *Wape chakula kizuri* Give them healthy food
Nguo za kuwasitiri And proper clothes;
Wapokowe' wanawiri Wash them so that they may shine
Ulinde yao afi ya And to protect their health.
- 1 -pokowa Am. "to wash" (Std. -ogeshu)
83. *Wana kula wahitaji* Children need food
Na ya kunwa safi maji And clean drinking water.
Afiya bora haji Good health does not come
Illa kwa kuizengeya Unless you make an effort.

90. *Mai sana ni muhimu* Water is of utmost importance
Kwa sisi wana adamu For us human beings.
Sipende mno ya tamu Don't give too much preference to juice;
Yalo swafi angaliya Look for clean water.
91. *Wana wape mai swafi* Give your children clean water.
Wala sambe mbona sifi Don't say, "Why? I have not died
Nami hunwa mai ghafi From drinking dirty water
Nyaka toka nyaka ngiya Year in and year out."
92. *Yuwa wana ni dhaifu* You should know, children are sensitive;
Tumbo zao ni khaifu Their intestines are feeble.
Mai yakiwa machafu When the water is dirty,
Mara huzuwa balaya It can cause sudden problems.
93. *Na uchafu si tototo* And this dirt is not a mud puddle
Kuwa taona kwa mato That you can see with the naked eye;
Kuna zilulu zitoto There are tiny bacteria
Kwazo maradhi heneya Through which sickness spreads.
94. *Zitutu mno zibombwe¹* These germs are so tiny,
Ukiteka kwa kikombe When you scoop up water in a cup,
Huziyoni nazo kumbe You cannot see them.
Zimo tele huoweya But—alas—plenty are swimming in it.
- ¹ *kibombwe* (pl. *zibombwe*) Am. "tiny germ."
95. *Hizo mno ni khatari* They are so dangerous;
Watu sana hukhasiri They harm many people.
Sharuti kutahadhari You must be careful;
Mara hukushambuliya They attack you suddenly.
96. *Maradhi yakimswibu* If sickness befalls the child,
Mwana yangawa hububu Even if it is a small thing,
Fanya kula taratibu Make every effort
Penye dawa kutapiya To run to a health center.

97. *Uwee siudharau* Don't ignore illness;
Mtoto huwa mkuu A small thing can grow big,¹
Ukawa na wayukuu And can be passed to grandchildren
Na zitukuu zikaya And even great-grandchildren.
- 1 An illness that is not cured can have long-term effects.
98. *Na mwana kiwa huhara* And if children have diarrhea,
Mpe mai kulla mara Constantly give them water,
Na dawa zilizo bora And don't delay
Sichelewe kuzengeya Looking for good medicine.
99. *Hata kama hutapika* Even if they vomit after drinking,
Mpe mai kadhalika Continue giving them water.
Yangawa mengi hutoka Even if a lot comes out again,
Machache yatasaliya Some will remain.
100. *Mai yakiwa katiti* If the water is not enough,
Muilini ni mauti This means death for the body.
Bila ya mai huketi Listen, without water
Muda mrefu sikiya You cannot survive for long.
101. *Wana kupowa ilimu* Understand, to have an education
Ni haki kuu fahamu Is a great right for children.
Ilimu nguzo muhimu Education is an important pillar
kwa wana waadamiya For all human beings.
102. *Ilimu kitu dharura* Education of all kind
Kwa jamii yake sura Is absolutely necessary.
Ilimu akiba bora Education is a good investment
Ya mwana kumuwatiya To make for your child.
103. *Wana lazima wasome* Children must learn
Maarifa wayatume To gain knowledge;
Wayezi tufanye shime Parents, let us make an effort
Ilimu kuwapatiya To offer them education.

104. *Wana tuwasomesheni*
Uwinga tuepusheni
Wana tusimamiyeni
Kuwekeza sawa ndiya
 Let us teach our children
 To do away with ignorance.
 Let us support our children
